




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**WAKALA YA MABASI YAENDAYO HARAKA**



LAPF Tower, Ghorofa ya Pili, S. L. P. 724, Dar es Salaam, Tanzania

**Simu:** +255 22 2700280/486 **Fax:** +255 22 2700603 **B-Pepe:** info@dart.go.tz **Tovuti:** www.dart.go.tz

Aprili 11, 2019

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **KUBORESHWA KWA HUDUMA YA MABASI KATIKA MFUMO WA DART**

Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka -DART, inapenda kuujulisha umma kuwa leo, Alhamisi, tarehe 11 Aprili 2019, huduma ya mabasi katika mfumo wa DART kuanzia Kimara Mwisho hadi katikati ya mji na sehemu nyingine za mfumo, zimerejea katika hali ya kawaida. Kuboreshwa kwa huduma ya mabasi kumetokana na kukamilika kwa matengenezo ya baadhi ya mabasi yaliyokuwa yameharibika.

Kwa leo idadi ya mabasi yanayotoa huduma katika mfumo ni mabasi 115. Wakala unaendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa huduma ya mabasi inaboreshwa na kuondoa kero kwa watumiaji wa mabasi yaendayo haraka.

Tunawaomba radhi wateja wetu kwa usumbufu uliotokana na upungufu wa idadi ya mabasi uliojitokeza jana, Aprili 10, 2019 katika mfumo wa DART wakati wa asubuhi. Aidha, tunawashukuru sana kwa ushirikiano wenu.

Tunawashauri muendelee kutufuatilia katika mitandao yetu ya kijamii ya Twitter (@DARTMwendokasi) na Facebook (DARTMwendokasi) kwa habari mpya za kuboresha huduma zetu. DART ipo kwa ajili yako.

**Mhandisi Charles S. Ogare  
Kaimu Mtendaji Mkuu**